

# **Huzuni Kwa Ajili Ya Dhambi (Mourning For Sin)**

**Na**

**John Kombo**

**(Mourning For Sin)**

# **Huzuni Kwa Ajili Ya Dhambi (Mourning For Sin)**

**Na**

**John Kombo**

**August 20, 2014**

# Huzuni Kwa Ajili Ya Dhambi (Mourning For Sin)

*“Heri wenye huzuni; maana hao watafarijika.”* (Mat. 5:4). Kauli hii kutoka kwa Yesu ni kitu kinachochanganya kwa wengine na kwa wakati uo huo inawafariji wengine. Hataiavyo hii haihusu usafi wa mtu binafsi na kwa anayehisi kwamba maisha yamembadilisha kwa muda mfupi. Siyo huzuni wa asili kama inavyoelezwa katika Warumi 12:15 ambapo Paulo alindika, *“Furahini pamoja na hao wafurao, lieni pamoja na hao waliao”*.

Bwana wetu Yesu anaagiza aina ya huzuni ambayo mtu huwanayo wakati anapohuzunika kwa ajili ya dhambi aliyoifanya katika maisha yake. Mtu anapoelewa mafundisho ya Biblia kuhusu usafi wa uzima, atahuzunika kwa ajili ya dhambi zake. Daudi alionyesha maana yake vyema alipoandika, *“Ninakiri dhambi zangu; ninasumbuliwa na dhambi”* (Zab. 38:18). Urefu wa huzuni haikuishia kwa Daudi. Pia ilionyesha wakati Yoeli alipoandika Mungu akimsihi Isaya katika Yoeli 2:12-13: *“Hata sasa, Bwana anatangaza, mnirudie na mioyo yenu yote, kwa kufunga na kuomboleza na kuhuzunika toeni mioyo yenu na sio mavazi, mrudieni Mungu wenu, maana ni mkarimu na mwenye huruma”*.

Tunaweza pia kupata mfano mzuri wa kuhuzunika kwa ajili ya dhambi zetu katika Luka 18:13 mfano wa Mafarisayo na Watoza ushuru *“...Mtoza ushuru akasimama kwa mbali asiweze hata kuangalia mbinguni lakini akipiga kifua chake akisema, “Mungu nihurumie, mimi mwenye dhambi.”* Ili kuwa na wazo la ndani la huzuni mtu anatakiwa kujilinganisha mwenyewe na mfano wa maisha ya Kristo alipokuwa katika ulimwengu, na kujali kwake kwa kila mmoja ambaye ni mfuasi wake. Mwandishi wa Kiebrania anaeleza kujali kwake Bwana dhidi yetu kwa kusema, *“Hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuliana nasi katika udhaifu wetu, lakini alijaribiwa katika kila namna, kama ilivyo kwetu sisi, lakini hakutenda dhambi.”*

Baada ya kujifunza jinsi tunavyo paswa kuhuzunika juu ya dhambi zetu tulizozifanya katika maisha yetu, hatupaswi kuishia hapo. Hataiavyo, Biblia inatuambia kwamba tunapaswa kuhuzunika kwa ajili ya dhambi za wengine, huzuni kama hiyo inaweza kutusukuma kufanya uinjilist zaidi, kuwatafuta waliopotea kwa injili.

Ndugu, ninyi nyote na binafsi, tuna wajibu wa kupeleka ujumbe wa wokovu katika dunia, kwa sababu dhambi ambayo hatujasamehewa italetta ghadhabu ya wenye dhambi wakati ambapo hukumu itakapo kuja. Hataiavyo, sisi ambao tumepewa wajibu huo tunakataa dhambi za

wengine, au wanatafuta kujiokoa wenyewe, wakiathiriwa na chaguzi zetu. Kukataa agizo la Mungu ipo kama ilivyo, ni dhambi (Yakobo 4:17).

John Kombo

Nakuru, Kenya.







